OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI J. K. NYERERE,
S.L.P. 3084,

Simu. Na. 02751721 **MOSHI.**

Kumb.Na.JKNSS/J/2020 ……

JINA LA MWANAFUNZI: _____

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI J. K. NYERERE

MANISPAA YA MOSHI – 2020

1.0 Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule hii kwa Mwaka **2020.** Shule ya Sekondari J. K. Nyerere ipo umbali wa kilometa 2 Mashariki mwa Mji wa Moshi. Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2020.** Unatakiwa kuripoti Shule tarehe **11/01/220** saa 1:00 asubuhi

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:

(a) **SARE ZA SHULE**

WAVULANA -Suruali mbili **(2) rangi ya kijivu-** Sampuli ya kitambaa kinapatikana shuleni.

-Shati nyeupe mbili **(2)** mikono mifupi.

WASICHANA - Sketi mbili **(2) rangi ya kijivu-** Sampuli ya kitambaa kinapatikana shuleni.

Sketi iwe na marinda saba mbele na saba nyuma.

-Blauzi nyeupe mbili **(2)** mikono mifupi.

- Sampuli ya mshono itapatikana shuleni.

-Wanaovaa **Hijabu** iwe ndefu kufikia pindo la skiti la kiuno chako pia sampuli itapatikana shuleni.

(b) Rangi ya **Hijabu** ifanane na shati la Shule

(c) Sweta iwe inafanana na rangi ya sketi au suruali

(d) Sare ya Michezo: - T.Shirt ya rangi ya **kijivu** sampuli inapatikana shuleni.

(e) Viatu vyeusi vya kamba venye visigino vifupi na siyo raba

(f) Mkanda mweusi wa ngozi usio na bakoli kubwa, soksi nyeupe wote

(g) Wavulana vesti nyeupe

(h) Wasichana vesti nyeupe au nyeusi

Masomo yanayofundishwa hapa shuleni ni **Uraia, Kiswahili**, **Kingereza, Hisabati, Historia, Jiografia, Baologia**, **Fizikia, Kemia, Upishi, Uhasibu na Biashara.** Masomo mengine utaelekezwa hapa shuleni.

MAHITAJI YA MASOMO

(i) Begi la shule lisilo na **mapambo wala maandishi** - (mifuko ya plastiki / sokoni haitakiwi).
(ii) Madaftari **12** (counter book) quire 2 kuendelea
(iii) Kalamu za wino na risasi
(iv) Mathematical Set na Logarithm table
(v) Kamusi ya kingereza na kiswahili

NB: Shule haina uwezo wa kuwapa wanafunzi wote vitabu vya kutosha vya rejea hivyo unapaswa kujinunulia vitabu kila unapoona pana upungufu.

3.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

3.1 Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.

(c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya

Mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

(e) Kutunza usafi wa mwili na mazingra ya Shule.

(f) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa.

(g) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote.

(h) Ni marufuku mwanafunzi kupitia kwenye uzio wa Shule na geti dogo la Shule ya Msingi.

1.5 HESHIMA

(a) Wanafunzi wote hawana budi kuonesha heshima popote wanapokuwa shuleni au nje ya shule.

(b) Lazima mwanafunzi kuheshimu na kutii viranja na viongozi wengine.

(c) Wanafunzi hawana budi kupendana na kuheshimiana wao kwa wao.

(d) Wanafunzi waheshimu na kuwatii walimu na wafanyakazi wote.

(e) Ni lazima wanafunzi waheshimu viongozi wao wa Taifa na Umma kwa ujumla.

(f) Wanafunzi ni lazima waheshimu wageni wanaokuja shuleni na kuwasaidia.

1.6 USAFI WA TABIA

(a) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuvuta tumbaku ya aina yoyote.
Kutumia kileo cha aina yoyote, kuvuta bangi, kulewa, kuiba, na kutumia lugha chafu au lugha ya matusi.
(b) Ni marufuku kwa mwanafunzi kwenda kwenye majumba ya starehe na nyumba za wageni [Guest Houses]

(c) Mazoea ya kushirikiana baina ya wasichana na wavulana lazima yaepukwe, hapa shuleni, na nje ya Shule.

1.7 USAFI BINAFSI.

Ni lazima kila mwanafunzi awe nadhifu, anyoe nywele ziwe fupi, marufuku kwa wasichana **kusuka nywele,** kufuga ndevu kwa wavulana ni marufuku,. Kucha ziwe fupi bila rangi. Nguo ziwe safi na ziwe zimenyooka [zipigwe pasi, viatu viwe vyeusi vyenye visigino vifupi na kamba na sio raba.

NB: Ni marufuku wavulana kuvaa mlegezo, suruali fupi na vibamba vikionekana vinachanwa:- mzazi mkague mtoto wako kabla ya kumleta.

1.8 USAFI WA MAZINGIRA.

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kuweka eneo la shule na majengo ya shule katika hali ya usafi wakati wote. Uchafu au takataka ni lazima zitupwe mahali panapostahili [kwenye shimo la takataka]. Ni MARUFUKU kwa mwanafunzi yeyote KUANDIKA au KUCHORA kuta za majengo ya shule, samani za shule na maeneo mengine katika eneo la shule.

1.9 UTARATIBU WA MASOMO

Siku za masomo ni kila siku ya Jumatatu hadi Ijumaa. Mwanafunzi anatakiwa kufika shuleni saa moja (1:00) asubuhi kwa ajili ya "roll call", usafi na matangazo muhimu. Masomo ya darasani yanaanza saa moja na nusu (1:30) kamili asubuhi. Ni lazima mwanafunzi awahi ili kushiriki shughuli za nje na hatimaye kipindi cha kwanza cha masomo.

2.0 UMUHIMU WA KUJIFUNZA

Ni muhimu sana kwa mwanao kujenga tabia ya kujisomea na kufanya maandalizi ya masomo siku inayofuata. Nakushauri utenge saa mbili au zaidi kila siku ambazo mtoto wako anahitaji kujifunza na kufanya kazi za masomo alizopewa shuleni.

2.1 MAHUDHURIO

1. Ni lazima mwanafunzi awepo shuleni muda wote wa shule.
2. Ni lazima mwanafunzi awahi na kushiriki katika shughuli zote za shule kama kuitwa majina
3. (roll call), usafi wa mazingira, shughuli za uzalishaji mali, michezo n.k. – atakayekwepa ataadhibiwa vikali.
4. Mwanafunzi anatakiwa kuitikia mara moja na kukimbia mahali atakiwapo mara asikiapo kengele au mwito mwingine wowote.
5. Ni lazima mwanafunzi awahi shuleni katika tarehe zilizopangwa mwanzoni mwa kila muhula au mapumziko ya aina yoyote.
6. Ni lazima mwanafunzi AHUDHURIE vipindi vya dini vya DHEHEBU lake.
7. Mwanafunzi HARUHUSIWI kubadili dhehebu lake shuleni.

2.3 MUHIMU

1. Ruhusa ya kutokuwa shuleni siku moja au zaidi ni lazima itoke kwa **Mkuu wa Shule au Makamu wake. Mzazi aliyeandikishwa shuleni** ndiye anayeruhusiwa kumwombea ruhusa mwanafunzi na sio **mtu mwingine yeyote.**

2. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na vyombo vya mawasiliano shuleni – redio na simu za mikononi. vikikamatwa **HAVITARUDISHWA KABISA.**

2.4 JIVUNIE SHULE YAKO:

Tafadhali jitahidi kila mara kujivunia shule ambayo mwanao anasoma kwa kutaka kufahamu zaidi shughuli zake na kutoa michango ya mawazo wakati inapobidi. Tutafurahi kusikia kutoka kwako kuhusu mawaidha utakayoweza kutupa kuhusiana na uendeshaji wa shule hii. Na timiza wajibu wako kwa mtoto wako kwa pamoja tutaendeleza watoto wetu.

2.5 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ulevi wa aina yoyote
4. Uvutaji bangi au sigara
5. Kuanzisha au kushiriki katika mgomo, au fujo hapa shuleni
6, Kuharibu kwa makusudi mali ya shule, walimu, wafanyakazi au watu wengine.
7. Kuharibu kwa makusudi na kutoheshimu Bendera ya Taifa
8. Kupata mimba, kutoa mimba,au kumpa msichana mimba.
9. Kuoa au kuolewa
10. Kutohudhuria shuleni miezi mitatu mfululizo bila taarifa
11. Kukataa adhabu au agizo la Mkuu wa Shule
12. Kudharau au kukataa kushiriki katika shughuli za kujitegemea hapa shuleni
13. Kupigana au kumpiga mwalimu au mfanyakazi au mwanafunzi mwenzake.
14. Kupatikana na uhalifu au kumjeruhi mtu yeyote nje na ndani ya shule.

TANIBIHI: 01

Kutakuwa na kikao cha wazazi wote wa wanafunzi wa kidato cha **I – 2020** tarehe **07/01/2020 saa 2:00** asubuhi , **siku ya Alhamisi**. Fika bila kukosa kwa faida ya mwanao hapa shuleni.

TANIBIHI : 02

Pamoja na maagizo haya tunaambatisha yafuatayo:

- Fomu ya taarifa binafsi ya mwanafunzi ya kukubali nafasi ya masomo katika shule hii
- Fomu ya Daktari ya Kupima Afya.

KARIBU SANA J.K. NYERERE SEKONDARI – KWA PAMOJA TUTAKUWA NA MAFANIKIO BORA.

……

FLORIDA A. NGOWI

MKUU WA SHULE

HALMASHAURI YA MANISPAA MOSHI

SHULE YA SEKONDARI J. K. NYERERE

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI YA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

A: JINA LA MWANAFUNZI (ALILOFANYIA MTIHANI)

……

TAREHE YA KUZALIWA……..

MAHALI PA KUZALIWA (MKOA, WILAYA)…….....

URAIA: MTANZANIA/SI MTANZANIA……..

B: TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

JINA LA MZAZI/MLEZI…….
KAZI YA MZAZI/MLEZI……..

ANWANI YA MZAZI/MLEZI……SIMU YA BABA……
SIMU YA MAMA…….

C : KUKUBALI SHERIA ZA SHULE – MWANAFUNZI

Mimi ……nimezisoma na kuzielewa sheria za shule na ninaahidi kwamba nitakuwa nazitii sheria zote na maelekezo mengine yote nitakayopewa na walimu na viongozi wote wa shule.
Tarehe……..**Saini**……

D: MZAZI

Mimi ……nikiwa (Mzazi/Mlezi) nimesoma/nimesomewa sheria na maagizo ya shule yanayohusu mwanafunzi.
……..ninaahidi kutimiza wajibu wangu kama Mzazi/Mlezi wa mtoto huyo kwa kushiriki ipasavyo na kutimiza mahitaji yake ya shule.

Tarehe……..**Saini**……..

E. TAARIFA ZA SERIKALI ZAMTAA ANAKOTOKEA MWANAFUNZI

MTAA.....KATA.....WILAYA.....

JINA YA MWENYEKITI WA MTAA/KITONGOJI.....

J.K. NYERERE SEC. SCHOOL,
P.O BOX 3084,
MOSHI.

……/……./ 2020.

To The Medical Officer,

……..

……

……..

.....

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FORM

Please Examine……(Name of Student)
Who has been selected to join this school for his/her fitness as a student in the following areas; to be completed by a Medical Officer.

1. Eye sight……
2. Hearing……..
   ……..
3. ……..
4. Specimen (i) STOOL……..
   (ii) URINE……..
   (iii) BLOOD……
5. ATHMA/TUBERCULOSIS……
   ……
   ……
6. PREGNANCY……..
7. OTHER DISEASES……..
   ……

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a medical Officer)

I have examine the above and consider that he/she is physically fit as a student
Date …….. Signature……..

Station…….Designation……..